

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Kumb. Na.DCC/AC.66/1

Tarehe 30/01/2024

TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia uwepo wa ajira ya Mkataba kwa nafasi ya Meneja Msimamizi wa Miradi.

MENEJA MSIMAMIZI WA MIRADI: NAFASI (1)

1. Sifa za Mwombaji:

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45
- Awe na Elimu kuanzia Kidato cha Nne/Sita
- Awe na Shahada/Stashahada ya Uzamili ya Uhandisi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na aliyesajiliwa na Bodi ya Usajili wa Uhandisi (ERB)
- Awe amesimamia miradi mikubwa ya ujenzi yenye thamani kuanzia Milioni mia tano na kuendelea (aweke vielelezo)
- Kufanya kazi zaidi ya miaka mitatu katika Taasisi za Umma au Binafsi

2. Maslahi

- Atalipwa mshahara ngazi ya Mkuu wa Idara katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LSSE 1)
- Atalipwa stahiki ya simu, umeme na nyumba
- Atapewa usafiri wa kutumia katika kutekeleza majukumu yake

OFISI YA MKURUGENZI, 1 MTA A WA MISSION, S.L.P 20950, 11883 DAR ES SALAAM, SIMU NA 2128800, 2128805,
Tovuti: www.dcc.go.tz, Barua Pepe: info@ilalamc.go.tz

3. Kazi na Majukumu:

- Kufanya kazi za Uhandisi na Usimamizi wa Miradi yote ya Halmashauri
- Kutoa Ushauri na Usimamizi wa kazi za ujenzi wa miradi
- Kutayarisha taarifa za maendeleo ya miradi za kila mwezi, robo na mwaka
- Kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa na takwimu za kujenga/kukarabati majenzi mbalimbali ya Halmashauri

Maombi yaambatanishwe na:

- Nakala ya Cheti cha kidato cha Nne/Sita
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- Nakala ya vyeti vya Taaluma –Shahada/Stashahada ya Juu
- Picha 2 (Passport size)
- CV

Jinsi ya kutuma maombi:

Barua zote za maombi ya kazi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili na namba za simu za mwombaji, Barua Pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 14 Februari, 2024.


Jomaary M Satura
MKURUGENZI WA JIJI

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

Anuani ya kutuma Maombi:

Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam,
S.L.P 20950,
DAR ES SALAAM.

OFISI YA MKURUGENZI, 1 MTAA WA MISSION, S.L.P 20950, 11883 DAR ES SALAAM, SIMU NA 2128800, 2128805,
Tovuti: www.dcc.go.tz, Barua Pepe: info@ilalamc.go.tz